# Je, mtu anaweza kuzuia kupata mimba baada yakujamiiana bila kinga (kufanya ngono zembe) kwa mfano amebakwa?

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Kama umebakwa au kulazimishwa kujamiiana unaweza kupata huduma katika hospitali, kituo cha afya , zahanati au kutoka kwa mhudumu wa afya ambaye atakupatia vidonge vya dharura vya kuzuia mimba. Hivi ni vidonge ambavyo vinatumika ili kupunguza uwezekano wa kupata mimba kama ulijamiiana bila kinga, au umesahau kutumia njia yako ya uzazi wa mpango au ulilazimishwa kujamiiana.

Ili ufanye kazi, njia hii ya dharura ya kuzuia mimba inatakiwa itumiwe ndani ya saa 120 (ndani ya siku tano) baada ya tukio. Inakuwa vizuri zaidi kama njia hii ya dharura itatumika punde bila kusubiri kwani kwa kufanya hivyo, ufanisi wake unakuwa wa kuaminika zaidi.

Hii njia ya dharura inazuia tu mimba kutungwa, haiwezi kusababisha kutoka kwa mimba pindi mimba ikishatunga. Utakapotafuta msaada wa kupata huduma ya vidonge vya dharura vya kuzuia mimba hasa kwa wale waliobakwa au kulazimishwa , mwombe mhudumu akusaidie kupata huduma ya kuzuia maambukizo ya UKIMWI. (Post exposure prophylasis). Unaweza kupata taarifa zaidi kwa mtoa huduma wa uzazi wa mpango kwenye kliniki za serikali, kliniki za UMATI, kliniki za Marie Stopes au sehemu yoyote wanapotoa njia za kisasa za uzazi wa mpango.